**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA PILI

## KIKAO CHA TISA

**12 FEBRUARI, 2021**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________________

## MKUTANO WA PILI

## KIKAO CHA TISA – TAREHE 12 FEBRUARI, 2021

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**114. MHESHIMIWA SIMON SONGE LUSENGEKILE (BUSEGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itapeleka Vifaa Tiba katika Hospitali ya Wilaya ya Busega ili huduma bora za afya ziendelee kutolewa.

**115. MHESHIMIWA ZAYTUN SEIF SWAI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kutokana na changamoto za vyanzo vya mapato hususan katika Halmashauri zilizo nje ya Miji

kumekuwa na uwiano usio sawa wa utoaji wa mikopo:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kutafuta njia ya kuweka uwiano sawa wa mikopo hiyo bila kujali mapato ya Halmashauri husika.

**116. MHESHIMIWA ZACHARIA PAULO ISSAAY (MBULU MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Mwaka 2015 Serikali ilitangaza kugawa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu na kupitia Vikao vya Mabaraza ya Madiwani wa Halmashauri za Mbulu Wilaya na Mbulu Mji walipitisha rasmi mgawanyo wa rasilimali na madeni: -

Je, ni lini Serikali itarejesha tamko la mapendekezo hayo ili kufanikisha maendeleo ya mambo yaliyopendekezwa.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**117. MHESHIMIWA DEUS CLEMENT SANGU (KWELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro wa ardhi uliopo katika Vijiji vinavyozunguka Hifadhi ya Pori la Akiba la Uwanda.

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

**118. MHESHIMIWA DAIMU IDDI MPAKATE (TUNDURU KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Jimbo la Tunduru Kusini limepakana na nchi ya Msumbiji kwa upande wa Kusini:-

Je, ni lini Serikali itafungua Ofisi za Mamlaka ya Mapato (TRA) Lukumbule.

**119. MHESHIMIWA STELLA SIMON FIYAO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kuondoa kodi kandamizi kwa Wafanyabiashara na kuweka kodi rafiki ili kuwasaidia kufanya biashara kwa uhuru na kulipa kodi kwa wakati na kuondokana na sintofahamu ya Wafanyabiashara kukimbilia kufanya biashara nje ya nchi.

## WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

### 120. MHESHIMIWA DOROTHY GEORGE KILAVE (TEMEKE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:- Serikali ilitenga eneo la Kurasini EPZ tangu mwaka 2014 kwa ajili ya uwekezaji lakini hadi sasa eneo hilo halijaendelezwa kama ilivyokusudiwa:-

Je, kwa nini Serikali isilirejeshe eneo hilo kwa Halmashauri ya Temeke ili lipangiwe shughuli za maendeleo.

## WIZARA YA KILIMO:

### 121. MHESHIMIWA HAWA SUBIRA MWAIFUNGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia Wananchi wa Tabora kuwa na soko la uhakika la zao la Tumbaku.

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuruhusu soko huria kwa zao hilo ili Wakulima wanufaike.

**122. MHESHIMIWA JOSEPHINE JOHNSON GENZABUKE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutafuta soko la uhakika la mazao ya Mahindi, Maharage na Mihogo.

**WIZARA YA MAJI:**

**123. MHESHIMIWA BRYCESON MAGESSA TUMAINI (BUSANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Mradi wa Maji wa Chankorongo utawekewa vituo vya kuongeza kasi ya maji ili upate uwezo wa kutoa huduma katika maeneo mengi zaidi Jimboni Busanda.

**124. MHESHIMIWA GEORGE NATANY MALIMA (MPWAPWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo la muda mrefu la uhaba wa maji kwa Wananchi wa Mji wa Mpwapwa.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**125. MHESHIMIWA FLORENT LAURENT KYOMBO (NKENGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini barabara za Kabyaile/Ishozi – Njiapanda ya Gera; Minziro – Mutukula; Kaja – Hospitali ya Mugana (Bwanjai) zitatengenezwa ili kuondokana na kero zinazowapata Wananchi wanaotumia barabara hizo.

**WIZARA YA NISHATI:**

**126. MHESHIMIWA VITA RASHID KAWAWA (NAMTUMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusambaza umeme wa REA kwenye baadhi ya Vitongoji vya Vijiji vya Namtumbo.

**III. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:**

***(Kusomwa Mara ya Kwanza)***

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2021 *[The Written*

*Laws (Miscellaneous Amendment) (No. 2) Bill, 2021].*

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu wa Mwaka 2021 *[The Accountants and Auditors (Registration) (Amendment) Bill, 2021].*

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2021/22 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2021/22.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA** — **S. KAGAIGAI**
**12 FEBRUARI, 2021** — **KATIBU WA BUNGE**